**BADILIKO**

Acha Badiliko Lianze na Mimi.

**Katika Kumtazama Tai**

Baadhi ya tai huishi kwa muda mrefu . Kama tai akigundua kwamba mabawa yake yanadhoofika anao uwezo wa kunyonyoa manyoya yake yaliyozeeka. Kwa kawaida sehemu zilizotoka manyoya katika kipindi cha miezi sita hupona. Ili kuweza kufika sehemu za juu zaidi na kuweza kuhuisha nguvu zake tai yuko tayari kubadilika. Wanaweza pia kukung'uta midomo yao iliyochongoka na kuota mingine.

**"Aushibisha mema uzee wako, ujana wako ukarejeshwa kama tai" (Zaburi 103:5)**

**"Bali wale wangojao Bwana watapata nguvu mpya; watapanda juu kwa mabawa kama tai; watapiga mbio wala hawatachoka; watakwenda kwa miguu wala hawatazimia (Isaya 40:31)**

Neno **"upya**" katika andiko hili linaweza kutafsiriwa **"Badiliko"**. Wale wanaomgojao Bwana nguvu zao zitabadilika. Badiliko hili linafanana na tai katika kupukutisha manyoya yake yaliyozeeka na kuota mapya.

Tai alikamatwa na kuwekwa kwenye banda pamoja na kuku. Alikaa pamoja na kuku na kufikiria kama wao. Alikua pamoja na kuku na kufikiria kama wao. Aliweza kutembea katika sehemu hiyo akidonoa donoa vipande vya makombo ya chakula na kula mara kwa mara, akiangalia juu angani na kuoona ndege wakiruka juu angani.

Siku moja kuku-tai akamwona tai akiruka juu.Kila siku alianza kuwaona wale wengine na kupigapiga mabawa yake. Aligundua kwamba mabawa yake yana nguvu zaidi kuliko wale kuku wengine. Siku moja aliinuka kutoka ardhini. Alipoendelea kupaa kwa mkazo alisema, kwaherini kuku! Hamtaniona tena. Nalidanganywa kwa muda mrefu, walakini sasa najua mimi ni tai."(imenukuliwa kutoka katika kitabu Money Cometh.) Kuku-tai alipaa upesi kwa sababu alikuwa tayari kubadilika.

## Kupaa Juu Kufanikiwa

Unataka kufanikisha nini katika kipindi cha uhai wako? Ni nini unalolifanya leo ili kuwezesha hili kutokea?

David McNally anapendekeza ujiulize maswali marahisi mawili kila siku kabla ya kwenda kulala.

1. Kwa leo mimi, kwa namna fulani, nimekuwa kama mtu?

2. Mimi kwa leo, kwa namna fulani, nimefanya ulimwengu kuwa mahali panapofaa kuishi?

3. Mimi kwa leo, kwa namna fulani nimefanya maendeleo kwa ajili ya kile ninachotaka kifanikisha katika kipindi cha uhai wangu?

4. Je! Nimelifanya kanisa kuwa mahali pazuri kwa ajili ya roho; na kwa ajili ya kizazi kijacho?

Unaweza kuwa umesikia wimbo unaimbwa **“Bwana tuma uamsho (revival) na uanze ndani yangu**

Angalia neno **“Revival”** lina herufi saba **“Revival” “Uamsho”** Ni herufi gani iliyo katikati ya **“revival”** Wakati ninapoanza badiliko inatakiwa ianzie ndani mwangu (wewe). Watu husema pia kwamba maombi hubadilisha mambo” Lakini katika maisha wanatakiwa wakubali kwamba; **“maombi hunibadilisha mimi!”**

“Maombi yanaweza yasibadilishe mambo kwa ajili yako, lakini ni hakika kwamba hukubadilisha wewe kwa ajili ya mambo.” Paulo alipoomba ili mwiba wake uondolewe, alimwomba Mungu kubadilisha mambo” Badala yake, Mungu akambadilisha ili aweze kuchukuliana na maumivu yake ya mateso. (Mwandishi wa makala haya hajulikani.)

Katika shirika lenye mafanikio wa kwanza kubadilishwa ni kiongozi. Mara kiongozi atakapotambua ilivyo vigumu kufanya mabadiliko katika maisha yake atajua vilivyo vigumu kufanya mabadiliko katika maisha kwa wengine. **John Maxwell** anadai “**badilisha kiongozi, badilisha shirika”** Dale Gallowa yanasema **“Jenga viongozi na viongozi watajenga huduma,”** Kabla shirika halijaenda kwenye hatua nyingine ya maendeleo lazima abadilike. Kila kiongozi mwenye ufanisi atakuwa na hamu na kukazana kuelekea maendeleo ya kudumu. Viongozi wazuri hudumu kuendelea kukua.

**“Howard Hendricks** katika **“Mafundisho kubadilisha maisha,”** anasema **“Kadri unavyobadilika ndivyo unavyokuwa chombo cha mabadiliko katika maisha ya wengine.**

**Kuendelea kwenye kiwango kinachofuata.**

Ili kuendelea kwenye kiwango kingine cha kanisa lazima kuwa tayari kukubali badiliko. Badiliko linatakiwa kwa ajili ya mafanikio.

**John Maxwell** alinukuu habari katika kitabu cha **Paulo Wharton** kiitwacho **“Habari ya mifano kwa ajili ya Wahubiri na Waalimu”** (Stories for Preachers &Teachers)

**“Nilikuwa mtu atakaye kugeuza kabisa kijana na maombi yangu yote kwa Mungu yalikuwa,’ Bwana nipe nguvu ya kubadilisha ulimwengu’ Nilipofikia umri wa kati na kugundua nusu ya maisha yangu yameondoka pasipo kubadilisha roho moja, nilibadilisha maombi yangu kuwa: ‘Bwana nipe na kubadilisha wote wanakuja kukutana nami, familia yangu na rafiki zangu, nami nitatosheka’ Sasa hapo ni mtu mzee na siku zangu zimehesabiwa. Nikaanza kutambua nilivyokuwa mjinga. Ombi langu moja sasa ni ‘Bwana nipe neema kubadilika binafsi.’ Endapo ningekuwa nimeomba maombi haya sahihi tangu mwanzo, nisingekuwa nimepoteza maisha yangu.**

Lifikirie. Ni muda gani unaoutumia kufikiri au kuzunguzia jinsi wengine wana weza kuendelea na /au badiliko? Kuwekeza wakati kuliko bora na jitihada zinaweza kutekelezwa kwenye kubadilika binafsi.

Gandhi aliwahi kusema. **“Uwe badiliko unalotaka kuona ulimwenguni.”** Leo Tostoy aliwahi kusema **“Kila mtu anafikiria kuubadilisha ulimwengu, lakini hakuna anayefikiria mwenyewe kubadilika.”**

**Kutoka Saauli hadi Paulo**

**"Lakini simama uingie mjini nawe utaambiwa ya kutenda" (Matendo 9:6) ".....nikijitahidi sana katika kuyashika mapokeo ya baba zangu" (Wagalatia 1:4)** Paulo alikuwa mwamini mzuri kwa badiliko lililowezekana. Siyo kwamba tu alijitahidi kuyashika mapokeo alikuwa ameshikwa nayo.

Habari ya Sauli inaanza na **"akazidi kuwaza kuwaua wanafunzi wa Bwana" Matendo 1:4)** na **nikawaua watu wa njia hii hata nikawaua, nikiwafunga nikiwatia gerezani wanaume na wanawake." (Matendo 22:4)** Kupitia vitendo vyake alitumaini kuwabadilisha Wkristo kurudi kwenyemapokeo ya kiyahudi. Kidogo sasa alikuwamo kwa ajili ya badiliko; (badiliko kubwa) Kuanzia hapo habari yake ikaanza kubadilika kuonekana amebadilishwa na kuwa ameangushwa chini, akitetemeka,mshtuko, kupofushwa, na asiyejiweza akisubiri katika Njia Kuu. (Kwa bahati mbaya sana baadhi ya watu wanahitaji kuangushwa chini kabla fahamu zao hazijafunguliwa.)

Wakati Sauli alipokutana na Bwana, aliuliza **"Bwana unanitaka nifanye nini?** inawezekana ikatamkwa kwamba Bwana unataka nibadilike vipi? **(Matendo 9:6)**

**Badiliko la imani kwenye barabara iendayo Dameski lilimleta Paulo kwenye njia iitwayo "Nyofu"** na kwenye safari iitwayo **"Badiliko"**

Mara Sauli alipobadilika alikuwa na ya utayari ulio bora kuwasaidia wengine katika hali ya kuendelea. Katika siku ya Pentekoste wale waliokuwa wamekusanyika waliuliza; **"Tutendeje ndugu zetu? (Matendo 2:38)** Hawa watu walitambulika kwamba walihitaji badiliko. Walichomwa mioyoni mwao. Kimsingi waliuliza "**Jinsi gani tunaweza kubadilika? "**

Hakuna hata mmoja wetu aliye mkamilifu. Yako maeneo katika maisha yetu ambayo yanahitaji kubadilishwa tunapokazana kwa ajili ya ukamilifu. Hatujawa jinsi ambavyo tunatakiwa kuwa, tutakavyo kuwa, au kuwa. Lakini kwa neema ya Mungu tuko ambavyo tumekuwa.

**Wote tunahitaji kubadilika**

**"Si kwamba tumekwisha kufika, au nimekwisha kuwa mkamilifu; la! Bali nakaza mwendo, ili nipate kulishika lile ambalo kwa ajili yake nimeshikwa na Kristo. Ndugu sijidhanii nafsi yangu kwamba nimekwisha kushika; ila natenda neno moja tu; nikiyasahau yaliyo nyuma, nikiyachuchumilia yaliyo mbele. Nakaza mwendo , nifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu. Basi sisi tulio wakamilifu na tuyawaze hayo; na hata mkiwaza mengine katika jambo lolote, Mungu atawafunulia hilo nalo." (Wafilipi 3:12-15)**

**Kuendelea Mbele**

H. S. Vigeveno anadai "Dr. Elton Trueblood anasema kwamba aidha kanisa lazima liendelee au lififie. Kundi lolote linalogoma kukua na kujieneza tayari linakufa. Kusimama mahali pamoja hakika ni Kifo na Kuoza.

*Unahitaji mwenyewe kujiuliza maswali matatu.*
}Ni nini linatakiwa lifanyike ili kuendeleza kanisa mbele?
}Ni nini ambalo wengine wanatakiwa kufanya kufanikisha hili?
}Mimi mwenyewe binafsi nitakwenda kufanya nini kusaidia kufanikisaha hili?

**Kuendelea ni kubadilika; kuwa mkamilifu ni kubadilika daima." (Wiston Churchill)**

Kuweza kufanikiwa katika kuubadilisha ulimwengu tunatakiwa kujifunza mawazo mapya. Tunatakiwa kudumu katika kujiendeleza.

Moja ya njia bora ya kutia changamoto ni kujenga mazingira ya ubora. **"Kuanzisha utaratibu wa maendeleo bora, fanya utakaloweza, unachoweza, mahali unapoweza." (Five Star Church)**

Stephen Covey anatoa ushauri wenye maana anaposema tunazo nafasi mbili. Tunaweza kuweka mtazamo katika upeo wa uwezo wetu; au kuweka mtazamo katika vitu ambavyo viko nje ya mtazamo wa upeo wetu. Wakati tunapoweka mtazamo katika yale yaliyo kwenye uwezo wetu tunakusudia kufanya maendeleo na kukamilisha malengo yetu. Walakini, wakati tunapoweka mtazamo wa mambo yale yaliyo nje ya uwezo wetu, kwa kawaida hatuwezi kufanya lolote kuhusiana nalo na kuishia katika manung'uniko na kutoa lawama.

Unapotazama katika kanisa yako mambo mengi yanahitaji kubadilishwa. Haihitaji kipawa karama maalumu kugundua maeneo haya na hata kuona makosa katika kanisa. Inahitaji kupambanua kuliko maalum kujua nini la kufanya kama suluhishi kwa matatizo. Mtu mmoja alisema **"Usije kwangu kuniambia juu ya matatizo endapo kwa wakati huo huo huwezi kunieleza ufumbuzi.**

**Mng'ato Mmoja kwa Mara Moja**

Ili kuweza kuona mabadiliko yanatokea katika kanisa. Inatakiwa ianze nawe na mimi. Hatua nyingine katika kuleta mabadiliko kutafuta eneo la kanisa linalohitaji badiliko tunaloweza kushikilia na kulifanyia kazi.Huwezi kuleta badiliko katika kanisa lote kwa mara moja lakini unaweza kufanyia kazi kwenye eneo moja la badiliko hadi litakapokamilika. Hili litakuendeleza wewe, maisha katika kanisa, na litawatia changamoto wengine kujihusisha katika badiliko.

**Kujihusisha kidogo mwenyewe inamaanisha kujihusisha mwenyewe katika swala lisilopo" (Michael LeBoef)**

Unamla tembo? Huli mga'to kwa mara moja. Safari iliyo ndefu huanza na hatua moja. Hatua ya kwanza inatakiwa ianze Siyo rahisi kufanyia mabadiliko kila kitu kwa mara moja.

**Nukuu katika Badiliko**

**"Sisi ni kile tunacho-rudiarudia kufanya. ubora, basi, siyo tendo, bali ni tabia." (Elmer Towns)**

Katika utangulizi wa somo ilitajwa, **Mambo sahihi hufanywa kwa kurudia rudia zaidi kufanyiza mafanikio."** Ili kwamba sisi tuweze kuwa katika ubora wetu, na kufikia ushawishi wa juu zaidi lazima tuwe wa kimataifa na wa daima. Tunafanyia kazi katika badiliko kila siku-Daima.

**"Maandalizi ya leo, yanaamua mafaniko ya kesho."**

**"Ni moja ya fidia ya maisha haya kwamba hakuna yeyote anayeweza kumsaidia mwingine pasipo kujisaidia mwenyewe." (Ralph Waldo Emerson)**

Kuanzisha tabia mpya (badiliko) **Dona Fisher** katika kitabu chake, **Nguvu ya Watu,** anapendekeza;

# Kuwa na utahadhari wa hitaji la kubadilika na hamu kubadilika.

# Chagua vitendo vipya, tabia, na mwenendo.

# Weka juu yake mtazamo na chombo cha kazi

**Kwa nini Watu Wanapinga Badiliko.**

**"Enyi wenye shingo ngumu,msiotahiriwa mioyo wala masikio, siku zote mnampinga Roho Mtakatifu; kama baba zenu walivyofanya, na ninyi ni vivyo hivyo." (Matendo 7:51).**

Kwa kurudia rudia, katika hizi Injili na Matendo ya Mitume Mafarisayo walikataa badiliko. Walikataa kuyaacha mapokeo yao. Kwa hakika Mafarisayo hawakuwa peke yao. Watu kwa nyakati zote wamepinga badiliko. Kwa nini?

Tom na Joani Schultz anatoa maoni katika kitabu chake. **"Kwa nini hakuna Yeote anyejifunza Kanisa Kwa Lolote: Na Jinsi Gani Inalitengeneza"** ni kwamba watu kadhaa wanakataa badiliko. Wanajumuisha:

**# Wameridhika.** Wanaridhika na pale walipo na wamekulia hilo kidesturi. Wametosheka.

**# Wamekosa ufahamu.** Hawafahamu tatizo au ufumbuzi. Wala hawaelewi ni jinsi gani mapendekezo ya mabadiliko yatakavyoweza kufanya kazi.

**Hawako tayari kulipa gharama.** Lazima waelewe hitaji la badiliko lakini hawaamini kwamba ina thamani kuwekeza muda au ni matatizo.

# **Wamefungwa ki-mapokeo.** Wimbo wao waliouzoea, **"Hivyo ndivyo tumekuwa tukifanya mara kwa mara."**

**# Hofu ya hasara.** Watapoteza nini kama mabadiliko mapya yatafanywa.

**John Maxwell** katika kitabu chake, **Kumwendeleza Kiongozi Ndani Yako** anaongeza orodha ifuatayo.

~ **Mazoea yanaingiliwa.** Badiliko huwa yanatishia mazoea yaliyofanya
.
**~ Badiliko linaanzisha hofu ya asiyejulikana.**

**~ Kusudi la badiliko siyo wazi.**

**~ Badiliko linasababisha hofu ya kushindwa.** Watu wanafikiria kwamba hawawezi kulifanya au kwamba litakwama.

**~ Tuzo la badiliko haliwiani na jitihada zilizohitajika.**

**~ Badiliko kamwe haliwezi kutokea wakati watu wakiwa na mawazo tofauti.**

~ Badiliko linaweza kupingwa kwa sababu **wafuasi hawana imani na heshima kwa kiongozi anayefanya mabadiliko.**

~ **Badiliko linahitaji zaidi kujihusisha.** Watu wanaweza kufikiri kwamba hawana muda unaohitajika kuletabadiliko katika eneo husika.

**Badiliko Ni Lazima**

Re. Richardson alisema,"**Endapo sisi, kama kanisa tutainuka kwenda kiwango kingine, lazima kuweko badiliko. Lazima tuwe tayari kubadilika."**

Imewahi kusemwa, **"Barabara ya kuelekea kiwango kingine mara zote ni kilimani"**

Badiliko siyo rahisi. Msimamo wetu wa mambo lazima uonyeshe utayari wa kubadilika ili kuweza kufikia kufanikisha mafanikio katika kukua kwa kanisa.

Wapi tunapoanzia badiliko? Hatua ya kwa ni **"kuanza tu.** Tendo linahitajika Anza leo. Kesho itakuwa imechelewa sana.

**Umuhimu wa Badiliko Ndani ya kanisa Leo.**

**"Maana tumemsikia akisema kwamba Yesu huyo Mnazareti atapaharibu mahali hapa, na kubadili desturi tulizopewa na Musa" (Matendo 6:14)**

**Huanza Na Badiliko**

Taratibu zote za wokovu ni utaratibu wa badilko. Mungu anatarajia mabadilko katika vitendo vyetu na tabia. (huitwa toba). Toba (repentance) linatoka katika neno la Kigiriki lenye maana **"badili kuonekana kwako nje"** au **"badilisha nia yako."** Hii inahusisha badiliko la akili, makusudi, na katika jinsi ile ambayo mtu anavyofikiria.

**"Basi zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni, bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu." (Matendo 17:30).**

TunapotubuYeye hutupa badiliko katika maisha yetu kwa kutusamehe, kuosha dambi zetu, na kutujaza sisi Roho Mtakatifu.

Yakobo na malaika usiku mmoja alipigana mwereka na malaika na akapokea jina kubadilika. Mungu alilibadilisha jina lake kuwa Israeli likimaanisha, "ameshindana na Mungu" Jina lake jipya linaelezea uhusiano wake mapya na Mungu. Mungu habadilishi jina la kila mtu lakini mara zote badiliko huusika.

**"Hata imekuwa mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama; yamekuwa mapya." (2 Wakorintho 5:17)**.

**Ukiri Huleta Mabadiliko**

| | |
|---|---|
| **Badiliko la Moyo** | Inahusisha toba na badiliko la tabia |
| **Badiliko la Maongozi** | Yesu Kristo sasa ni Msimamizi mwenyewe. |
| **Badiliko la Uaminifu** | Kujishughulisha kabisa katika kumtumikia Yesu. |

**Badiliko la Mfumo wa Maisha** Kupata kumfahamu Mungu.

Hivyo, tukio letu lote la ukristo huanza na badiliko. Pia litaishia na badiliko. Hudhanii kwamba kutakuweko na mabadiliko kadri muda unaovyoendelea pia?

**“Atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, uweza ule ambao kwa huo aweza kuvitiisha vitu vyote viwe chini yake.” (Wafilipi 3:21)**

**Inatakiwa. Umuhimu wa Badiliko.**

Leo, kanisa linahitaji kuzalisha viongozi wapya. Ni moja ya vianzo vyenye kuhitaji upambanuzi sana. Kwa kanisa kuendelea , sisi , kama viongozi lazima tunahitaji kwanza kuendelea. Huweka mfano na kuwekeza katika maisha yake mwenyewe kifaa cha mabadiliko. Imewahi kutamkwa **“Kiongozi yule anayeongoza, huendelea.”** Kabla ya kutarajia wengine kukua, kwanza lazima tukue. **Howard Hendricks** alisema, **“Kama unapenda kuendelea kuongoza, lazima uendelee kubadilika.”**

Katika nyakati za **“hakukuwa na badiliko,”**usimamizi tu, ukarabati na mapokeo na matengenezo huweka magurudumu ya shirika hufanya mwisho wa kazi. Katika nyakati za **“mabadiliko”** uimara na kuanzisha mwazo mapya) kuanzisha jambo jipya (kuweka mawazo mapya katika matumizi) maongozi yanahitajika. Mawakala wa badiliko huzalisha huanzisha mawazo mapya yatakayotia changamoto badiliko na kufanya kadri wawezavyo kuhamasisha kukubalika kwa ajili ya hayo mabadiliko kutoka kwa wengine. Hii inataka kupenda, tabia ya uvumilivu na mawasiliano ya wazi.

**Badiliko katika Kitabu cha Matendo.**

Kitabu cha Matendo ya Mitume ni kitabu cha Badiliko.**Commentary ya The Life Aplication** inasema Kitabu cha Matendo kinaweza kuitwa **“Miujiza ya Maisha yaliyobadilishwa.”** Nyaraka zilifungwa na wanafunzi wakikimbia kuponya maisha yao. Katika kitabu cha Matendo tunaona watu kwa ujasiri wa kitangazaInjili. Kulikuweko na badilisho ambalo Mungu alilitumia kuubadilisha ulimwengu. Anataka kufanya kitu cha jinsi hiyo hiyo kupitia kwetu leo.

Pentekoste ilileta badiliko la nguvu sana na kuwafanya watu kuuliza,**”Tutendeje ndugu zetu?” (Matendo 2:12).** Maisha yalibadilishwa kupitia ubatizo wa Roho Mtakatifu na ubatizo wa maji katika jina la Yesu. Maisha ya nyumbani yalibadilishwa pale chumba kilipoandaliwa kwa ajili ya waamini wapya. Mahali pa kukutania palibadilika pale tu waamini walipoanza mkutano nyumba kwa nyumba. Mfumo mpya wa kutoa ulianza pale pale washirika walipouza mali zao na kuleta fedha kanisani.

Hatimaye, mateso yakaleta badiliko kadri waamini walivyotawanyika kila mahali. Mtazamo mpya kiakili ulihitajika ili kuwapokea mataifa waamini (walioonekana ni kisichoguswa kwa Wayahudi) Baraza katika Yerusalemu lilileta badiliko katika kuleta matarajio katika waamini. Watu wakuu walibadilika kwa nguvu kama Paulo. Hatimaye alitumika kama wakala wa badiliko kuanzisha mwenendo wa kimisionari.

Katika Matendo 6 viongozi hawakuweza kuendeleza huduma ya kimitume kwa sababu walikuwa wakisubiri mezani. Ililazimu kubadili na kuweka sawa kulingana na vipao mbele. Hata siku za leo wahubiri wanafanya mambo mengi ambayo kwa urahisi tu yangeweza kushughulikiwa na washirika na viongozi wa mahali husika.

Petro aliwaasa makutano katika siku ya Pentekoste ku **“jiokoa wenyewe na kizazi hiki chenye ukaidi” (Matendo 2:40)** Alikuwa anaelezea kizazi kisicho na mwelekeo. Walikuwa wanazunguka zunguka katika gurudumu la mapokeo.

Mara kwa mara Mitume walibadilisha mfumo watu walivyozoea (walivyotenda mambo). Walikuwa tayari kuupindua ulimwengu (Matendo 17:6). Walitambulisha njia mpya. **“Wanasema kwamba kuna mfalme mwingine, aitwaye Yesu” (Matendo 17:7).** Walishtakiwa kwa kuhubiri Yesu.

**“Maana tumemsikia akisema kwamba Yesu huyo Mnazareti atapaharibu mahali hapa, na kuzibadili desturi tulizopewa na Musa (Matendo 6:14).**

***Yesu, Mungu Abadilishaye lakini Bado Habadiliki Kamwe.***

Tunatakiwa tuwe mawakala wa badiliko. Tunahubiri Injili ambayo ni ujumbe ubadilishao maisha. Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuwa mawakala wa badiliko. (Mathayo 23:1-23; 5:21-44)

Katika Mathayo 5, Yesu alikuwa juu mlimani akitoa “**sifa za uheri”** kwa watu Wake. Alitamka mara kadhaa, **“Mmesikia kwamba wa kale walivyoambiwa usi…” (Mathayo 5:21).** Na baadaye akafuatia kila wakati kusema **Bali mimi nawaambia....(Mtahayo 5:22)** Alikuwa anajaribu kubadilisha desturi za mawazo. Walakini, watu huwa wana kawaida ya kushikilia mapokeo.

**“Akawaambia Vema! mwaikataa amri ya Mungu na kuyashika mapokeo yenu. Huku mkilitangua neno la Mungu kwa mapokeo yenu mliyopokeana,tena mwafanya mambo mengi sawa sawa na hayo (Marko 7:9,13).**

***Baadhi ya Mambo Mengine Kabisa Hayabadiliki*.**

Ni sharti la mapito ya zamani zinapofikia kwenye Mafundisho ya msingi. **“Bwana asema hivi?simameni katika njia kuu, mkaone, mkaulize habari za mapito ya zamani, I wapi njia iliyo njema? Mkaende katika njia hiyo, nanyi mpatajipatia raha katika nafsi zenu. Lakini walisema Hatutaki kwenda katika njia hiyo. (Yeremia 6:16)**

**“Hatimaye, ndugu zangu, furahini katika Bwana. Kuyaandikieni mambo yale yale hakuniudhi mimi, bali kutawafaa ninyi. (Wafilipi 3:1).**

**“Nastaajabu kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kuigeukia Injili ya namna nyingine: Wala si nyingine; Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni watawahubiri ninyi yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri na alaaniwe. Kama tulivyotangulia kusema, na sasa, nasema tena, mtu yeyote akiwahubiri ninyi Injili yoyote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe” (Wagalatia 1:6,8-9).**

Tunaendelea kuhubiri ujumbe **“huo huo”** Injili na kuinua mafundisho ya Biblia na taratibu. Walakini, mbinu lazima zibadilike kuendana na nyakati zinazobadilika. Ulimwengu unaotuzunguka daima hubadilika. Tunamtumikia Mungu asiyebadilika katika ulimwengu unaobadilika-badilika..

**“Yesu Kristo ni yeye yule jana, na leo, na hata milele” (Waebrania 13:8)** (Yeye kamwe Habadiliki; sisi tunabadilika)

**“Kwa kuwa Mimi BWANA, sina kigeugeu” (Malaki 3:6)**

Yesu alikutana wana desturi katika siku Zake, walioitwa Mafarisayo. Walishikilia katika njia za zamani na kukataa kuchukuliana na mabadiliko Yesu aliyoyatetea. Yesu daima aliendelea kupingwa kwa sababu alitetea mabadiliko. Alitaka badiliko la mawazo, badiliko la moyo, na badiliko la mfumo wa maisha. Moja ya adui mkubwa kwa kanisa leo inaweza lisitoke nje. Inaweza kuwa **“desturi,”** usisitiziaji wa kufanya namna ile ile iliyokuwa inafanyika miaka iliyopita. Kuleta hisia ya kuwa salama, mara kwa mara inaitwa “**ukanda wa faraja.”** Endapo jinsi mambo yanavyotendeka kazi inatendeka, idumishe. Kama haifanyi vizuri leo, na tuwe jasiri kiasi cha kubadilika.

**“Kama mara zote utakuwa ukifanya ambacho umekuwa ukifanya mara kwa mara, utakuwa ukipata ambacho umekuwa ukipata mara zote.” (John Maxwell)**

Ni rahisi kutambua hali ya kimapokeo katika wengine, Lakini kuiona katika maisha yetu wenyewe ni vigumu zaidi.

Tunahitaji kutembea katika mafundisho ya awali na kuishi maisha ya kitauwa.Katika maeneo mengine tunahitaji kuchimbua njia mpya za kuanzisha badiliko. Njia za zamani haziwiani tena hali mpya. “Imewahi kutamkwa , **“Hakuna hali iliyo ya kudumu”.** Hali hubadilika. Uchaguzi lazima uchunguzwe na tahadhari kuchukuliwa. Hata katika miili tunaweza kuona kuwa wote wanaokua hubadilika.-hukua. (Mwili katika hali ya **aging**)

Dan Reiland katika “**Pastor’s Coach” (December 2000)** alitaja mambo manne ambayo kabisa hayabadiliki. Aliongeza:

1. Hamu ya kufahamu na kufahamika; kupenda na kupendwa.
2. Msukumo na hamu ya kuunganika na muumba wetu.
3. Hitaji kwa ajili ya uongozi wa kiroho.
4. Bidii na hamu kufanya jambo lenye maana kabla maisha yetu hayajafikia ukingoni.
5. Matazamio ya amani, ridhaa na furaha katikati ya shinikizo na machafuko.

***Hitaji kwa ajili ya Mawakala wa Badiliko.***

Kama viongozi tunatakiwa tuanzisha hisia kuona busara ya badiliko.Tunawatia changamoto wengine kuona hitaji la badiliko la aina hiyo. Kuwa na mtazamo katika faida ipendezayo kutoka katika badiliko linavyofanya hili. Lazima tuweze kuwajibu. ”**Kwa nini hili ni bora kwako”**

**Thom na Joani** pia alitoa maoni **mpango kwa ajili ya mawakala wa badiliko.**
Mpango huu unajumuisha:

**>Elezea hitaji.** Watu wamejawa na tabia  za zamani na njia zao. Watahitaji kufahamu tatizo.

**>Weka mtazamo kwenye faida zitakazopokelewa  pamoja na hitaji ulazima wa badiliko.**
Watu wengi huwa wanafikiria watakachopoteza kwa badiliko jipya. Badala yake lazima usaidie kwenye mtazamo wa watakacho-faidika.

**>Uelewe kwamba siyo kila mmoja atafurahia badiliko.** Huweza kumpendeza kila mmoja. Mafanikio yote kufanywa pamoja na watu na ukorofi wa-watu kupinga.

**Usijaribu kuweka kazi ya mabadiliko yote kwa wakati mmoja.** Waongoze watu wako moja kwa moja katika badiliko hatua moja baada ya nyingine.

Inawezeakana pia kuongezewa: **Wape watu umiliki wa badiliko. Waonyeshe watu jinsi badiliko litakavyo wafaidisha.**

***Kutafuta Mwakala wa Badiliko zaidi***

Nyakati za mabadiliko kunatakiwa kuwepo na hitaji la msisitizo mpya katika huduma ya mwili. Washirika wetu wanatakiwa wachukue jukumu la mwili (kanisa)

"**Kama desturi ya kusanyiko fulani katika hali ya kutokuwa na nafasi ya watu kujaribu kutumia karama zao, basi desturi zetu na zisambaratikie mbali vipande vipande! Na tutazame muundo mwingine ambao utakuwa na uwezekano wa watu wa Mungu kutumia vipawa vyao. Kama desturi zetu zinamaanisha mtu mmoja aendeshe basi na kila mmoja nyuma ni abiria nyuma, tunatakiwa tukumbuke kwamba kanisa linafananishwa na mwili, siyo basi. Siyo kwamba ni dereva mmoja tu na wengine wote mmekaa nyuma mkiburudika nyuma wakimpigapiga mabegani dereva kwa kumpongeza kumhakikishia anafanya kazi nzuri na kwamba yeye anatakiwa aendelee. Ni nini tunalolifanya kuhakikisha washirika - washirika wa kawaida-wamegundua karama zao na kwamba njia imefanywa wa wao kuweza kufanyia kazi hizo karama ili ziweze kuwafaidisha wote. Ni viongozi wangapi ambao watakuwa wanajisaidia wenyewe kutokana na vidonda vya tumbo, uchovu na hatari ya mashambulizi ya moyo endapo watayapuuza mashauri ya Yethro?"**

Nukuu hii inamwelezea mshirika ambaye atakuwa anajishirikisha ndani ya **"huduma ya mwili."** Kila mshirika anayo sehemu ya kushughulika katika mwili wa Kristo.

Elton Trueblood aliwahi kusema **"walio chini (washirika) siyo abiria kwenye merikebu. Wao ni washirika katika kundi."**

*Kubadilisha Mawakala katika Shirika la zamani.*

Kuwa wakala wa badiliko katika shirika lililopangiliwa vizuri siyo rahisi. Mhariri **Randall Roberts** katika kitabu, **Kutoka Somo la Maongozi: Kwa heshima ya Stahiki** anataja vidokezo kadhaa jinsi ya kuwa wakala wa badiliko katika huduma iliyopangiliwa vizuri.

* **Mara zote hifadhi sifa njema ya wakati uliopita.** Daima sifia na kamwe usiwashutumu viongozi waliopita. Msingi waliouweka ni urithi ambao kiongozi aliyepo anaoufurahia. Kama viongozi waliotangulia bado wako hai wahabarishe maendeleo. Uwape usikivu maalumu.

* **Nenda taratibu.** Inachukua miaka kumi kufanya mabadiliko makubwa katika shirika la zamani. Usifanye mabadiliko makubwa mwaka wa kwanza. Uwafahamu watu na historia ya hilo shirika.

* **Tafuta msaada mpana kwa ajili ya badiliko.** Jaribu kupata kuungwa mkono kwa ajili ya badiliko. Ufanye kila mmoja kuelekea mwelekeo mmoja.

* **Badiliko ni maumivu.** Uwe tayari kwa maumivu. Siyo rahisi kufanikisha lengo.

* **Toa mawazo yako yaliyo bora zaidi.** Waruhusu watu wako wafikie wajisikie kuwa kama mawazo hayo ni ya kwao. Panda mbegu katika kila mkutano.

* **Toa changamoto, tia moyo, mvike kila uwezo kila mtakaye fanya kazi naye..** Kabisa usitosheke na kiwango cha chini walakini utafute ubora zaidi.

**Andaa mawakala wa badiliko kukufuatia wewe.** Washauri wale watakaokuwa mawakala wa badiliko kwa kizazi kingine.

* **Angalia nyuma.** Unahitaji kufahama umefikia wapi ili kwamba uweze kujua utaekwenda umbali gani. (Vidokezo hivi vimetolewa katika waraka wa barua pepe iliyokuwa na kichwa cha habari **Marupurupu ya Huduma-Kuimarisha Huduma Yako.**

***Kazi ya kufanya***

Orodhesha maeneo matano unayopenda kuona yamebadilika katika maisha yako.
1.______________________________________________________________________________
2..______________________________________________________________________________
3.______________________________________________________________________________
4.______________________________________________________________________________
5.______________________________________________________________________________

Orodhesha maeneo matatu ya kanisa unayoweza kutumiwa ili kuleta mafanikio, badiliko halisi:
1.______________________________________________________________________________
2..______________________________________________________________________________
3.______________________________________________________________________________